Sikika

Jarida la Sikika

Namba ya Usajili 00005809 Toleo 23: Septemba 2016

Huduma Bora za Afya kwa Wote

SAM Yaanza kwa Mafanikio Kilolo

Emmanuel Malongoza, Kilolo

Zoezi la Ufuatiliaji na Uwajibikaji kwa Jamii (UUJ/SAM) limewawezesha wananchi na uongozi wa halmashauri ya Kilolo kufahamu kwa kina changamoto zinazoikabili sekta ya afya na kutoa mapendekezo ya kuboresha huduma za afya wilayani humo.

Utoaji na upatikanaji wa huduma za afya wilayani Kilolo unakabiliwa na changamoto hasa katika baadhi ya vituo vya kutolea huduma za afya vilivyotembelewa na timu ya SAM. Miongoni mwa changamoto hizo ni ukosefu wa vichomea taka, upungufu wa mashimo ya kutupia kondo la uzazi, kushindwa kumalizia baadhi ya miradi ya afya hususan majengo ya zahanati licha ya jitihada za wananchi kujenga hadi kufikia kiwango cha lenta.

Changamoto zingine ni uhaba wa watoa huduma za afya na ukosefu wa maji ya uhakika katika vituo vya kutolea huduma za afya. Vilevile, timu ya SAM iligundua kuwa kuna umbali mrefu kati ya baadhi ya vijiji na zahanati au vituo pamoja na matatizo ya usafiri hasa katika maeneo ya pembezoni mwa wilaya hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kilolo, Mh. Valence Kihwaga alikiri uwepo wa changamoto hizo na kuomba ushirikiano wa wadau wote pamoja na serikali kuu ili kuzitatua. Kuhusu majengo ya vituo vya afya kutomalizika baada ya wananchi kujenga mpaka kwenye lenta na hivyo serikali kushindwa kumalizia alisema “sera ya serikali ilisema wananchi wajenge maboma wakifikia kwenye lenta serikali imalizie...magofu yaliyopo ni kielelezo kuwa sera ya serikali haijafikiwa. Hivyo, tusaidiane kwa pamoja kutoa taarifa serikali kuu ili tupate msukumo wa juu, haya maboma yaweze kukamilika.”

Kuhusu changamoto za utoaji huduma, Mh. Kihwaga alitoa wito kwa watoa huduma za afya kufanya kazi kwa uwazi na kushirikisha wananchi katika maeneo yao. “...hii dhana ipo isipokuwa watu wanafika mahali wanafanya kazi kwa mazoea, hilo ndio tatizo kubwa. Timu ya SAM na Sikika wametoa msukumo na chachu kwamba watu wasijisahau, watekeleze majukumu yao ya kutumikia wananchi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.”

Mwenyekiti Kihwaga pia alitoa pongezi kwa timu ya SAM na waratibu wa mafunzo kwa kusema; “Sikika wamekuwa tofauti na mashirika mengine...walipokuja ofisini kwangu nilitaka kusita pale waliponiambia wanataka nyaraka za Serikali/Halmashauri huku nikifahamu nyaraka za serikali zina miiko... lakini kumbe shirika lina mpango mzuri wa uwazi wa utekelezaji wa mambo ya umma hasa yanayohusu jamii na kuboresha huduma za afya”.

Akizungumzia mafunzo na ziara ya timu ya SAM, Mwenyekiti wa timu hiyo, Bw. John Kasuga anakiri kuwa yamesaidia jamii pia kuelewa changamoto hizo, wajibu na umuhimu wa kufuatilia na kushiriki katika shughuli za maendeleo, “Tusiwe tunasubiri serikali ije ituboreshee huduma za afya, mambo mengine yamo ndani ya uwezo wetu…tuyafanyie kazi ili kuboresha huduma, pazuri tupaendeleze na pabaya tupaboreshe.”

“Tunapenda ushauri kutoka kwenu Sikika na timu ya SAM... tunaahidi ushirikiano wa kutosha kwa timu ya SAM pamoja na shirika la Sikika, wananchi wajitoe ili kufanikisha maeneo ya uboreshaji yaliyobaki tusiiachie serikali tu...wajumbe mkafanye kazi ili huduma bora zipatikane”. Anamalizia Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri Mh. Mejusi Mgeveke.

Timu ya SAM ya Kilolo iliipongeza Halmashauri na watoa huduma kwa jitihada kubwa zilizofanywa kwa upande wa usafi kwenye vituo vya afya karibu vyote. Timu ilipendekeza serikali kuu isaidie kutatua changamoto hizo kwa kutenga na kutoa kwa wakati bajeti ya kutosha katika sekta ya afya nchini.

Mafunzo hayo ya SAM yaliratibiwa na Sikika na kutekelezwa na timu ya wawakilishi wa wananchi 15 kutoka katika makundi mbalimbali ya jamii wilayani Kilolo.

Wajumbe wa timu ya SAM wilayani Kilolo wakikagua moja ya ujenzi wa Zahanati katika zoezi la SAM lililofanyika Wilayani humo.

NDANI

SAM Yaanza kwa Mafanikio Kilolo 1
Wananchi Wadai Huduma za Afya 2
Serikali Yakataa Mapendekezo ya UN 3
Mazingira ya Kazi Bado Changamoto 4

HALIUZWI

Wananchi Wadai Huduma za Afya

Na Thomas Ludovick, Kondoa

UKOSEFU wa zahanati katika kijiji cha Mongolo wilaya ya Kondoa, mkoani Dodoma umewafanya wananchi wa kijiji hicho kupata adha ya upatikanaji wa huduma bora za afya na kuwalazimu wanakijiji kutembea umbali mrefu ili kutafuta huduma hiyo.

Hayo yalibainika hivi karibuni katika ziara ya tathmini iliyofanywa na timu ya Ufuatiliaji na Uwajibikaji kwa Jamii (UUJ/SAM) kwenye vituo vya afya na zahanati katika Halmashauri ya wilaya hiyo. Hali hiyo inatokana na kutokamilika kwa ujenzi wa zahanati ya Mongolo kwa zaidi ya miaka 20 sasa kutokana na mgogoro uliopo kati ya wananchi na viongozi wa halmashauri ya Kondoa.

Chanzo cha mgogoro huo kimetokana na halmashauri ya Kondoa kuwashauri viongozi wa kijiji cha Mongolo kuvunja jengo la zahanati hiyo kutokana na jengo hilo kujengwa kwa kutumia ramani ya zamani. Hali iliyosababisha wananchi kuzua mgogoro mkubwa kutokana na kufanya jitihada za kujitolea fedha zao wenyewe na kujenga zahanati hiyo hadi kufikia hatua ya lenta.

Akizungumzia suala hilo katika mkutano wa wadau wa afya kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji na Mkuu wa Wilaya ya Kondoa Bw. Abubakari Kuuli anasema inasikitisha kuona wananchi wanachanga fedha zao kwa ajili ya kujenga zahanati na baadae wanaambiwa ramani waliotumia sio sahihi, hali hii inapelekea kuwavunja wananchi moyo katika kuchangia miradi ya maendeleo.

“Mimi binafsi nilifika nikajionee ila tutafika kwa mara nyingine tena na timu yangu ili kuongea na wananchi wa pale… kama tutakubaliana kuongeza vyumba kwenye jengo lile lile au kuifanya kuwa nyumba ya watumishi na pembeni yake tukaanza ujenzi wa zahanati mpya.” Anasema Bw. Kuuli.

Awali akiwasilisha taarifa ya zoezi hilo katika mkutano wa wadau wa afya uliofanyika wilayani humo, mjumbe wa timu ya SAM, Bw. Omari Saidi anasema wakiwa katika ziara ya kutembelea zahanati mbalimbali wilayani humo, walikuta ujenzi wa zahanati ya Mongolo haujakamilika tangu mwaka 1994.“Ujenzi huu haujakamilika kwa muda mrefu kutokana na kuwa katika mgogoro wa kuendeleza jengo hili. Hali hii inapelekea wananchi wa hapa kukosa huduma za afya, hivyo kuwafanya kutembea umbali wa kilometa 5 hadi 6 kutafuta huduma za afya katika kijiji jirani cha Itololo,” anasema Bw. Saidi.

Akifafanua, Mganga Mkuu wa wilaya ya Kondoa Dk. Rashid Ikaji anasema ujenzi wa zahanati katika kijiji cha Mongolo unatakiwa kuanza upya kwa kufuata ramani ya sasa inayokidhi mahitaji. Hivyo Halmashauri itafanya ukamilishaji pale jengo litakapofikia hatua ya lenta.

“Hata hivyo itategemeana na upatikanaji wa fedha….kama Halmashauri tuliwashauri kuvunja kwa sababu ramani imepitwa na wakati, tuliwapatia ramani mpya ya ujenzi wa zahanati itakayokidhi mahitaji ya sasa. Tutafika tena na kuona namna gani ya kuitatua changamoto hii,” anasema Dk. Ikaji

Pia, baadhi ya wananchi wa kijiji hicho wameelezea kukata tamaa kutokana na kuchoshwa na ahadi za baadhi ya viongozi wanaotoa ahadi bila kuzitimiza kwa muda mrefu sasa. “Wananchi wa kijiji hichi tumechanga fedha zetu wenyewe na kusimamisha jengo hili hadi hatua ya lenta, lakini hadi sasa serikali haionyeshi nguvu za kuimalizia, tumekuwa ni watu wa kudanganywa…viongozi wanakuja kuomba kura wakipata wanaondoka hatuwaoni,” anasema Bw. Hassan Bakula.

Baadhi ya wananchi wa kijiji cha Mongolo wilayani Kondoa na wajumb haujakamilika k

“Akinamama wakati wa kujifungua tunapata shida kubwa ya kutembea umbali mrefu, kipindi cha masika mito hujaa maji, hivyo tunashindwa kwenda kupata huduma za afya kijiji jirani na wengine kujifungulia njiani…tunaomba serikali itusaidie akinamama tunateseka mno.” Anasema Bi. Khadija Chonde.

Serikali Yakataa Mapendekezo ya UN

Na Mariagoreth Charles

Serikali imeyakataa mapendekezo ya nchi nane wanachama Umoja wa Mataifa (UN) yaliyolenga kuboresha utekelezaji wa haki ya kupata taarifa nchini. Mapendekezo hayo yaliitaka serikali kuhakikisha Sheria ya Vyombo vya Habari (MSB) inatoa haki ya kujieleza kama ilivyo katika mikataba ya kimataifa, kuhakikisha Sheria ya Haki ya Kupata Taarifa inafuata misingi ya kimataifa ya haki za binadamu, kuboresha sheria zote zinazovunja haki ya kujieleza mathalan Sheria ya Takwimu (2015), Sheria ya Uhalifu wa Mitandao (2015) pamoja na Sheria ya Magazeti (1976).

pe wa timu ya SAM wakikagua ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho ambao wa muda mrefu.

Hayo yalifahamika wakati wa maadhimisho ya Siku ya Haki ya Kujua (Right To Know), yaliyofanyika jijini Dar es Salaam Septemba 28, mwaka huu. Mapendekezo hayo yalitolewa na nchi za Jamhuri ya Czech, Denmark, Ubelgiji, Sweden, Marekani, Uingereza na Ireland ya Kaskazini, Uholanzi na Ureno na kufanyiwa tathmini ya utekelezaji wa haki za binadamu (UPR) huko Geneva, Uswisi.

Ilielezwa kwamba pendekezo pekee lililokubaliwa na serikali ya Tanzania ni lile lililotolewa na nchi ya Australia linaloitaka serikali kushughulikia malalamiko yanayohusiana na madai ya kuingiliwa kwa uhuru wa kujieleza.

Akifungua warsha hiyo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Mh. Amos Mpanju alisema "…kwenye kukataa mapendekezo kunakuwa na sababu nyingi … sisi kama serikali lazima tuhakikishe mapendekezo hayo yanaenda sambamba na sera za nchi, sheria za nchi, katiba ya nchi, mila, utamaduni na maadili ya taifa".

Mratibu wa zoezi la UPR kutoka Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Bw. Deogratius Bwire alitoa ufafanuzi kwamba watetezi hao wamekuwa wakisisitiza serikali ikubali mapendekezo yote ya haki ya kupata taarifa kwa vile wakiyakataa, baada ya miaka minne serikali haitowajibika kuonesha ni namna gani imeboresha mapendekezo hayo, bali itawajibika kwa pendekezo moja tu ililolikubali.

Moja ya sababu kuu zinazofanya wadau wa haki ya kupata taarifa kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa haki hii kwa kutumia taratibu za kimataifa ni kuwezesha wananchi kufahamu jinsi fedha zitokanazo na kodi zao zinavyotumika. Nyingine ni kuwakumbusha viongozi dhana ya uwajibikaji kwani uongozi ni dhamana waliyopewa na wananchi.

Katika maadhimisho hayo, Taasisi ya Habari Kusini mwa Afrika, tawi la Tanzania, (MISA-Tan) ilitoa tuzo zake maarufu zenye ishara ya Kufuli na Funguo. Wizara ya Katiba na Sheria ilipatiwa 'tuzo' ya Kufuli, ikiashiria kwamba taasisi hiyo ni chombo cha umma chenye usiri mkubwa wa taarifa za umma. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilitunukiwa tuzo ya Funguo kuashiria kwamba ni chombo cha umma chenye uwazi wa hali ya juu kati ya vyombo vyote ya umma vilivyofanyiwa utafiti na MISA-Tan.

Tunaamini kwamba haki ya kupata taarifa ikibanwa inaleta athari hasi kwa maendeleo. Uwepo wa haki ya kupata taarifa unakuza uwajibikaji katika utendaji, unaongeza ushiriki wa wananchi katika miradi ya maendeleo na hatimaye kuleta mabadiliko chanya.

Mazingira ya Kazi Bado Changamoto

Na Catherine Festo

Vituo vingi vya kutolea huduma za afya vinakabiliwa na changamoto ya kukosa mazingira bora na rafiki ya kutolea huduma. Hali hii husababisha watumishi wengi kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi na ustadi hivyo kuathiri huduma zitolewazo kwa wananchi. Changamoto hii ilionekana katika vituo vingi vya kutolea huduma za afya wakati wa tathmini ya utoaji wa huduma za afya uliofanywa na Sikika katika wilaya 20 nchini mwanzoni mwa mwaka 2016.

Lengo la tathmini lilikuwa kufahamu hali halisi ya upatikanaji wa huduma ya afya nchini ili kusaidia uandaaji wa mpango kazi wa Sikika 2016-2020. Moja ya changamoto iliyojitokeza hasa kwa maeneo ya vijijini ni majengo yanayotumika kutolea huduma kuchakaa bila kufanyiwa ukarabati hali ambayo si salama kwa watoa huduma na watumiaji.

Pia, kwenye baadhi ya maeneo, majengo yanatumika kutolea huduma wakati huo huo ni makazi ya watumishi. Kwa mfano, katika zahanati ya Kasangezi wilaya ya Kasulu, mkoani Kigoma, jengo moja linatumika kama makazi ya mtumishi, huku chumba kimoja katika jengo hilo kikitumika kwa shughuli za maabara, na kingine kutumika kulaza wagonjwa hasa akinamama na watoto pale wanapozidiwa.

Changamoto nyingine ni ukosefu wa miundombinu imara kama vile barabara zinazopitika majira yote. Katika baadhi ya maeneo, vituo vya kutolea huduma za afya havifikiki kipindi cha mvua. Kwa mfano, daraja linalounganisha kituo cha afya cha Mgori na hospitali ya wilaya ya Makiungu mkoani Singida hujaa maji wakati wa masika na hivyo kuathiri usafirishaji wa wagonjwa wanaopata rufaa. Hali hii huweza kuchelewesha wagonjwa kupata huduma na pengine kuleta madhara makubwa zaidi kama vifo, jambo ambalo lingeweza kuzuiliwa kwa kuimarisha miundombinu.

Ukosefu wa maji safi na salama katika maeneo mengi na hasa vijijini ni miongoni mwa changamoto ambazo zinaathiri utoaji wa huduma za afya kwa mfano katika zahanati ya Mpara, wilayani Kilwa watumishi na ndugu wa wagonjwa hutembea umbali wa zaidi ya kilomita 2 kutafuta maji ya kisima. Hii huwaongezea mzigo watumishi wa afya kwa kutumia muda mwingi kutafuta maji lakini pia hupunguza muda wa kutoa huduma kwa wagonjwa.

Changamoto nyingine iliyojitokeza katika vituo vingi vya kutolea huduma za afya hasa katika maeneo ya vijijini ni ukosefu wa vyoo bora, safi na salama. Vyoo katika vituo vingi vya kutolea huduma za afya havina paa imara, milango wala maji hivyo kuhatarisha afya za watumiaji.

Mazingira ya kufanyia kazi kama vile uwepo wa nyumba bora za watumishi, maji safi na salama, vyoo bora, miundo mbinu imara, mawasiliano na uwepo wa umeme ni jambo la msingi kwa mtumishi katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya. Vile vile ni motisha kwa mfanyakazi ili kumwezesha kudumu katika eneo lake la kazi.

Hivyo basi Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ifanye jitihada za dhati katika kuboresha mazingira ya kazi ili kuwapa motisha watoa huduma na kuboresha utoaji wa huduma katika vituo vya kutolea huduma vya umma.

Wananchi pia wana jukumu kubwa katika kuhakikisha wanaboresha mazingira ya vituo vya kutolea huduma za afya. Mathalan, kushiriki katika kuchangia ujenzi wa miundombinu ya kituo kama vile vyoo na mahali pa kuchomea taka hatarishi ili kuepuka milipuko ya magonjwa. Vilevile kamati za vituo zina jukumu la kuhakikisha mazingira ya vituo yanawezesha upatikanaji wa huduma bora za afya.

Mjumbe wa timu ya SAM wilayani Lindi mjini akikagua huduma za mnyororo baridi katika zahanati ya Narunyu. Kulia kwake ni Muuguzi wa zahanati hiyo.

Sikika

Nyumba Na. 69
Ada Estate, Kinondoni
Barabara ya Tunisia
Mtaa wa Waverley
S.L.P 12183 - Dar Es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 26 663 55/57
Ujumbe Mfupi: +255 688 493 882

Nukushi: +255 22 26 680 15
Barua Pepe: info@sikika.co.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Blog: www.sikika-tz.blogspot.com
@sikika1
Sikika Tanzania
sikikatanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani
S.L.P 1970
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 23 21307
Nukushi: 026 23 21316